BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Saba – Tarehe 22 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

151. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kupitia mkutano wa Umoja wa Mataifa uliojadili masuala ya tabianchi uliofanyika Dubai mwezi Disemba, 2023 (COP28), moja ya ajenda zake, ilikuwa ni kuongoza nchi zinazoendelea katika kukabiliana na athari za tabianchi kwa kuanzisha vyombo vitakavyodhibiti na kupunguza uzalishaji wa gesi chafu (greenhouse gas emission).

Je, Serikali imejiandaa vipi kutekeleza muongozo huo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

78. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wizi wa mazao umekuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi wa Zanzibar. Hali hii inatokana na kutopewa vibali wakulima wanapokwenda kuuza mazao yao sokoni kutoka shehia husika, tofauti na zamani walipokuwa wanapatiwa cheti cha mazao ikiwa ni utambulisho wa uhalali wa mazao yao.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi tatizo hilo.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wakulima hao.

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Imekuwa jambo la kawaida kwa wafanyabiashara wengi wanaotoa huduma za vyakula kushika na kuwahudumia wateja kwa kutumia mikono bila 'gloves' au visaidizi vya kushikia.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kupambana na tatizo hili ambalo linachangia sana kusambaa kwa maradhi mbali mbali nchini.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

30. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imeamua kuwapa mikopo wananchi wake ili waweze kujiendeleza kimaisha.

(a) Je, hadi sasa ni kiasi gani cha pesa kimewafikia walengwa.

(b) Kwa kuwa ule mgao wa 4.4.2 unaotokea Halmashauri sasa unaletwa Wizarani kwako, Je, pesa hizi nazo zimeshaanza kutolewa kwa wahusika.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

1. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililifanyia usafi bwawa la Mwanakwerekwe na kupelekea bwawa hilo kuwa na haiba nzuri na ya kupendeza.

   (a) Je, Serikali kupitia Mradi wa BIG Z ina mpango gani wa kuliendeleza bwawa la Mwanakwerekwe pamoja na mabwawa mengine kama vile bwawa la Ziwa Maboga na bwawa la Sebleni.

   (b) Je, kwa sasa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa mabwawa haya yanakuwa salama na kuvutia na sio hatarishi kwa maisha ya wananchi.

64. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Kumekuwa na malalamiko kuhusiana na mantiki ya misamaha ya kodi kwamba hakuna tofauti za kimsingi zinazoridhisha kiuchumi baina ya wale waliopatiwa na wale waliokataliwa.

   (a) Je, ni aina ipi ya miradi ya kijamii inaruhusiwa kusamehewa kodi kisheria.

   (b) Je, kuna tofauti gani za kikodi kati ya miradi ya kijamii inayosimamiwa na mpango wa TASAF na ile inayosimamiwa na mpango wa CDF.

   (c) Je, ni kwa utaratibu upi miradi ya kijamii kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) husamehewa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

18. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

   Kwa kuwa Serika imeimarisha sekta ya elimu kwa ujezi na ukarabati wa skuli mbali mbali nchini.

   Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika kuimarisha sekta

hiyo kwa jimbo la Wawi ndani ya miaka mitatu iliyopita.

54. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna ushahidi wa kitakwimu unaonyesha kwamba baadhi ya skuli za ghorofa zimejengwa sehemu zisizo na ulazima na kuziwacha sehemu zenye mahitaji ya lazima kwa ajili ya elimu ya maandalizi, msingi na sekondari.

(a) Je, ni ipi takwimu ya idadi ya wanafunzi katika skuli za ghorofa zilizojengwa mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024.

(b) Kwa kuwa katika jimbo la Pandani kuna skuli zenye mahitaji zaidi ya madarasa ya ziada, ni upi mpango mpya wa karibuni wa kupeleka madarasa ya ziada katika skuli hizo.

(c) Je, ni lini Serikali imekusudia kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa na walimu walioajiriwa katika skuli za jimbo la Pandani hasa skuli ya msingi ya Kiungoni.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

103. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Sanaa na maigizo ni miongoni mwa tasnia zinazotoa mchango mkubwa katika kuingiza pato la Taifa katika mataifa mbali mbali duniani.

Je, tathmini iko vipi hapa kwetu Zanzibar.

119. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na tatizo la ving’amuzi vya ZMUX kwa watumiaji wa Wilaya ya Mkoani na tatizo hili ni la siku nyingi sasa, mpaka watumiaji hao wamekata tamaa tokea mwaka 2022, japokuwa wengine wanaendelea kulipia.

(a) Je, ufahamu wa Wizara yako uko vipi juu ya tatizo hili.

(b) Ni lini Wizara yako italitatua tatizo hili.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tatizo la kuzagaa kwa mifugo mitaani limekuwa linaathiri jitihada mbali mbali za kiuchumi kwa wananchi wetu.

(a) Je, Wizara yako imejipanga vipi katika kuliondoa tatizo hili hususani kwa maeneo ya Uzi Bondeni, Magirisi, Nakivubo na kwa Mwarabu.

(b) Kuna taratibu gani za kisheria kwa mtu anaeathirika kwa kuvamiwa na mifugo eneo lake au bustani yake ya mboga mboga.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

116. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Zanzibar inasifika sana duniani kwa uzalishaji wa viungo licha ya kwamba uzalishaji wa baadhi ya viungo hivyo, ukitoa zao la karafuu, haujakidhi mahitaji ya soko la kimataifa.

Je, ni yepi matarajio ya Wizara yako katika kuhamasisha uzalishaji wa viungo nchini ili kukidhi soko la kimataifa.

**Wizara ya Afya:**

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ukosefu wa lugha za alama kwa madaktari unaleta usumbufu katika kuwahudumia ipasavyo watu wenye mahitaji maalum.

Je, ni upi mpango mkakati wa Wizara yako katika kuhakikisha kuwa kunapatikana wataalamu wa lugha za alama kwenye taasisi zote za kiafya nchini.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

145. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na utata kuhusu umiliki wa fukwe za bahari katika hoteli zilizopo pembezoni mwa bahari katika sehemu za Unguja na Pemba. Utata huu umesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaopita na wanaotumia fukwe hizi.

(a) Je, Serikali inayo habari kuhusiana na utata huo katika baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba.

(b) Ni hatua gani ambazo Serikali imezichukua katika kukabiliana na usumbufu unaowakumba wananchi wanaotumia maeneo haya ya fukwe.

(c) Je, mikakati gani iliyowekwa na Serikali kuhusu umiliki wa fukwe za bahari ili kuzuia migogoro na kuhakikisha haki za wananchi zinalindwa wakati wa kutumia maeneo hayo ya fukwe.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

24. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ni Taasisi inayotoa ushauri elekezi kwenye miradi mbali mbali ya ujenzi pamoja na ujenzi wa majumba. Lakini kwa masikitiko makubwa ni kuwa miradi mingi ya Serikali huwa hawapewi kuisimamia.

(a) Kwa kuwa Taasisi hii ina wataalamu waliobobea katika ujenzi, kwa nini Serikali haioni haja ya kuwapa usimamizi wa miradi ya Serikali wataalamu hao.

(b) Kwa nini Serikali haioni haja ya kuipa kazi Taasisi hii kuishauri Serikali kupitia miradi yake mbali mbali ili kuwa bora zaidi na kupunguza gharama za ziada za matumizi.

57. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na matangazo ya vyombo vya baharini vinavyolazimisha nauli za watoto ziwe kwa watoto wasiozidi miaka 10 badala ya miaka 18 ya kimataifa au miaka 12 ya

SUMATRA.

(a) Je, ni ipi mantiki ya kuwa na bei ya mtoto katika vyombo vya usafiri.

(b) Je, ni sheria ipi inayomtambua mtoto kwamba lazima asizidi miaka 10.

(c) Je, kwa nini Serikali haizielekezi mamlaka husika kuangalia uwezekano wa kuwa na punguzo la bei katika vyombo vya usafiri kwa wazee waliozidi miaka 70 na wanafunzi angalau wa skuli.

87. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara kuu na barabara za ndani (feeder roads). Lakini hivi sasa kumekuwa na changamoto ya barabara zilizojengwa ama kukatwa kwa shughuli za kimaendeleo au kujengwa matuta makubwa yasiyokuwa na vipimo ukilinganisha na gari zinazopita maeneo hayo na kusababisha gari hizo kukwaruza na kuharibika. Hali hiyo inajitokeza zaidi katika barabara ya Fuoni Mambosasa, Hawaii na juu ya kilima cha Kijichi.

(a) Je, ni sababu zipi za kimataifa zinazoifanya barabara kujengwa matuta.

(b) Je, kwa nini matuta katika barabara hizo yamejengwa makubwa ukilinganisha na mwinuko wa gari ndogo ambazo ndio nyingi zinazopita na huwa zinakwaruza.

(c) Je, ni lini mikato hiyo itazibwa kwani imekuwa ya muda mrefu na mingine ipo katika sehemu hatarishi zinazoweza ama kuharibu vyombo vyetu au kusababisha ajali.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):</u>**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2023/2024.

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**

**Zanzibar,**
**22 Februari, 2024.**